

**Appendix to „Bongo Flava and the Electoral Campaign 2005“**  
**by Uta Reuster-Jahn**  
*All song lyrics were transcribed and translated by Uta Reuster-Jahn*

**No. 1 *Kura yangu* – Dr. Levy & Sugu**

Yeah, we're talking HipHop here, tunazungumzia HipHop, kama muziki na maisha <sup>1</sup> , siasa ndani, Dokta Levy.	<i>Yeah,</i> <i>We're talking HipHop here,</i> we are talking about HipHop, as music and as life, politics within, Dr. Levy.
Kura yangu toka mikononi mwangu, napiga kumchagua kiongozi wangu, atakayeiongoza nchi yangu niliyopewa na Mungu. Ni kweli. Isiwe kura ya kula <sup>2</sup> nikapata hasara kwa kumchagua kiongozi aliyekosa busara. Noma! Tusiwe na mawazo fukara, tukageuza biashara zoezi la upigaji kura. Tusichague mradi chama tuangalie ubora wa sera.	My vote from my hands, I cast it to choose my leader who will lead my country which was given to me by God. It's true. It shouldn't be a "vote of eating", which would result in detriment, because of choosing an unwise leader. A shame! Let's not have destitute thoughts, and subsequently turn the voting exercise into business. Let's not choose just a party, but assess their policies' quality.
Eh mungu! Kura yangu, waondolee adhabu bibi na babu	Eh, God! My vote should remove the burden from grandmother and grandfather
ya kutembea maili nyingi kwenda kufuata matibabu, noma! Nikashindwa kumlaumu kata, waziri na katibu, kaka zangu ngoja nisiendeleo kuwasulubu. Uh! Ninapokwenda hospitali manesi wawe na adabu.	of walking many miles To seek medical treatment, a shame! I can't blame the ward, minister and secretary, my brothers, don't let me continue to aggrieve you. Oh! When I go to the hospital the nurses should behave properly.
Kura yangu iwapunguzie machungu moyoni ndugu zangu kufukuzwa machimboni. Salamu mpaka Mbuguni! <sup>3</sup> Noma!	My vote should alleviate the bitterness in the hearts of my brothers who were driven from the mines. Greetings to Mbuguni! A shame!
Mzawa kuondolewa mgeni anapokelewa. Miaka mitano mwanzoni ushuru kodi anafutiwa. Nisingependa mambo haya tuendeleo kutendewa. Kwa yeyote mwenye akili ninachosema anakielewa. Eheee.	The national is being removed, and the stranger welcomed. For the first five years he needn't pay taxes or customs. I would not like these things to continue happening to us. Everybody with a brain understands what I'm saying. Eheee.
Wanamuziki hatufiki tunakosa haki miliki.. Wabunge wetu watarajiwa kasemeni vikaoni. Kasemeni! Naamini hata nyie hampendi tushinde vijiwani. <sup>4</sup>	We musicians don't succeed 'cause we lack copy right. Our MPs, you are expected to speak out in the meetings. Speak out! I'm sure that even you don't like us to spend our time at the jobless youth's meeting places.
Acheni fikra potofu kwamba haki iko mbinguni	Forget the wrong thought that our right is in heaven.

<sup>1</sup> *Muziki na Maisha* is the title of an album released by Mr. II (one of Sugu's former names) in 2001.

<sup>2</sup> *Kura ya kula* ('a vote of eating') is a rhyming word-play connecting *kura* ('vote') and *kula* ('eat'). This saying alludes to the fact that votes are "sold" for small gifts like food, money, and the like.

<sup>3</sup> The name of a Tanzanite mining area south of Arusha.

<sup>4</sup> *Kijiwe* (literally 'little stone') is used in colloquial speech to denote the usual meeting place of groups of youth, mainly those who have no job (Reuster-Jahn & Kießling 2006: 131).

**Kiitikio:**

Kura yangu!  
 Nawauliza viongozi waliyesimama,  
 ni yupi kati ya wale waliobeba dhamana  
 aweze kutuongoza sisi kwa amani?  
 Maisha bora mijini na vijijini,  
 hakika sasa jibu ninalo kichwani:  
 Kura yangu!  
 Hakika sasa jibu ninalo kichwani:  
 Kura yangu!  
 Hakika sasa jibu ninalo kichwani:  
 Kura yangu!

Bado ninaendelea kusema.  
 Soko huria bado tatizo kwa wakulima.  
 Tuombe tuwe salama.  
 Yeee!  
 Tunajivunia amani viongozi ndivyo wanavyosema.  
 Uchaguzi unapokaribia wanarudi majimboni

kwenda kujipatia kura kwa blaablaa za mdomoni.  
 Noma!  
 Na vijisenti kidogo mfukoni kuwarubuni,  
 waweze kuchaguliwa warudi tena bungeni,  
 kwenda kupiga soga na kuingiza mamilioni.

Oooh!  
 Maisha ni duni, pesa inashuka thamani  
 tokea sitini, sabini, themanini mpaka tisini,  
 na sasa ni elfu mbili na bado tu yupo tu wizarani.  
 Wizarani!  
 Anapata shinikizo na mwongozo.  
 Tukapate kiongozi mwenye uwezo kifikra na  
 kimawazo.

Mungu ndiye mweza tunamtanguliza.  
 Tangulia!  
 Tujaliwe tupate kiongozi bora wa kutuongoza.  
 Nawaza kile nasema, nasema kile nawaza.  
 Ndiyo hivyo!  
 Tunataka utawala bora katika kila idara,  
 mahakama, wizara, kwenye mashirika mpaka jela.  
 Jela!  
 Mabadiliko ni ya lazima.  
 Oh!  
 Tusikubali kila kitu wanachosema  
 Ahaa!  
 Mahospitali na mashule ya binafsi ndiyo  
 yamechukua nafasi,  
 Na sasa sitakubali kura yangu kuiipoteza.  
 Noma!!!  
 Imetoshia nilivyojieleza kwa heri nimemaliza

Ni kama bado hujamaliza!  
 Naisha

*Chorus, aha!*

**Kiitikio****Chorus:**

My vote!  
 I ask the leaders who stand for election,  
 who among those who gave an election pledge  
 will be able to lead us peacefully?  
 A better life in the towns and villages,  
 sure, now I have the answer in my head:  
 my vote!  
 Sure, now I have the answer in my head:  
 my vote!  
 Sure, now I have the answer in my head:  
 my vote!

I'm still speaking.  
 The free market still poses a problem to peasants.  
 Let's pray to live in safety.  
 Yeee!  
 We are proud of peace, that's what our leaders say.  
 When the election comes near, they go back to their  
 constituencies,

to gather votes by blaablaa from their lips.  
 A shame!  
 And small money in their pockets to lure them [the voters],  
 that they might be elected and go back into parliament  
 to chat and pouch millions.

Oooh!  
 Life is low, money loses its value,  
 from the sixties, seventies, eighties till the nineties,  
 and now it's two thousand and he is still in the ministry.  
 In the ministry!  
 He gets pressure and guidelines.  
 May we get a leader with intellectual abilities.

God who is the Almighty, we let him lead the way.  
 Lead the way!  
 May we get a good leader to lead us the way.  
 I think this, I say that, I say this, I think that.  
 That's how it is!  
 We want a better administration in every department,  
 courts, ministries, in the companies up to the prison.  
 The prison!.  
 Changes are necessary.  
 Oh!  
 We should not accept everything they say.  
 Ahaa!  
 Private hospitals and schools have been started.

And now I will not agree to gamble away my vote  
 A shame!  
 I have now expressed myself sufficiently, good bye, I have  
 finished.

It is as if you had not finished!  
 I end here!

Chorus, ahaa!

**Chorus**

Wataka kura ndiyo wakati siyo – no!  
 Sikupi ndiyo wakati itikadi zako siyo,  
 na sera zako siyo  
 yaani kila kitu siyo!  
 Wanasisia wahuni ni lazima tuwafaini.  
 Hata kama mimi ni mwananchi masikini  
 kura yangu ina thamani  
 Sasa nishaelimika.  
 Sasa siyo kama zamani  
 sasa sitauza kura kwa pilau<sup>5</sup> kwenye sahani.  
 Kha!  
 Mtanzania mwenye nia kura yangu ina thamani  
 Nikikupa nataka elimu bora mashuleni  
 Halafu nataka dawa hospitalini  
 pembejeo za kutosha mashambani  
 na msaada kwa vijana wa mijini  
 kupambana na umaskini.  
 Halafu sitaki rushwa kabisa serikalini.  
 Tunaona kila idara rushwa bado inatawala.  
 Kura yangu simpi tena waziri wa ile wizara  
 alikuwa mlalahoi mchapakazi mara leo  
 mfanyabiashara,  
 na anavyozidi kuwa tajiri hali yangu inadorora.

Ah!  
 Kura yangu ndiyo silaha nitaitumiaje vema?  
 Labda nimchague mtu nisiangalie tena chama.  
 Haya shemeji kazi kwetu kina baba kina mama.  
 Wengi ni wale wale wa kampeni ya tisini na tano,  
 watasema yale yale mwaka elfu mbili na tano.  
 HipHop,  
 HipHop!  
 Yeah!

***Kiitikio***

You want a “yes” vote while it is “no” – no!  
 I don’t give you “yes” when your commitment is “no”,  
 and your policies are “no”,  
 in fact, everything is “no”!  
 The corrupt politicians, we have to punish them.  
 Even if I’m a poor citizen,  
 my vote has a value.  
 Now I have already understood.  
 This time it’s not like in the past,  
 this time I will not sell my vote for a dish of pilau.  
 Kha!  
 [I’m] a Tanzanian with a will, my vote has a value.  
 If I give it to you, I want good quality education in the schools.  
 Then I want medicine in the hospitals,  
 enough agricultural tools in the rural areas  
 and support for the urban youth  
 to fight poverty.  
 Then I don’t want any corruption in the government.  
 We see that in every department corruption is still ruling.  
 I will not again give my vote to that minister  
 who was an idler, then a worker and now a businessman,  
 and while he is getting richer all the time my living  
 conditions get worse.

Ah!  
 My vote is a weapon, how can I use it well?  
 Maybe I should choose a person without regard to the party.  
 Okay, brother-in-law, we have to tackle it, men and women.  
 Many of them are the same like in the campaign of 1995,  
 they will still say the same in 2005.  
 HipHop,  
 HipHop!  
 Yeah!

***Chorus***

<sup>5</sup> *Pilau* is a dish made from rice, meat, potatoes and spices.

## No. 2 *Tawile* 1 - Joni Woka

“Mama Salehe, ongeza sauti yaani volume kidogo kidogo!”	“Mama Salehe, crank up the voice, I mean the <i>volume</i> , a little bit!”
“Ehee.”	“Okay.”
“Mama Juma ee!”	“Mama Juma ee!”
“Be!” <sup>6</sup>	“Be!”
“Njoo, kuna jambo mie nataka kukuambia. Si unajua uchaguzi sasa umekaribia?”	“Come here, there is something I want to tell you. You know of course that the election has come close now?”
Na uongozi watu wengi wanauwania, na mimi madarakani mie sitaki kuachia, japo wananchi ahadi zao mimi sijawatimizia.	So, many people are striving for leadership, and I do not want to let off power, even if I have not achieved what I have promised to the citizens.
Sasa mie nani atanisaidia ili madarakani niweze kubakia.”	Now, who will help me to stay in power?”
“Mume wangu, kuna wazo moja ambalo limenijia, mganga <sup>7</sup> ndiye ambaye atakayekusaidia. Tena Mjalu, wengi amewasaidia, nenda mume wangu, nenda!”	“My husband, I have got an idea, it ‘s the medicine man who will help you. He is a Luo who has already helped many. Go, my husband, go!”
“Hilo hilo ndilo ninalokupendea Kichwa chako chepesi sana cha kufikiria. Poa, mama <sup>8</sup> , kwa mganga naelekea. Baadaye!”	“That’s why I love you, Your brain is very quick in thinking. Very well, Mama, to the medicine man I will go. [See you] later!”
Kiitikio: “Hodi mganga! Kwako mimi nimekuja mganga” “Pita ndani!” “Nisaidie mganga, madarakani nibakie, mganga” “We, pita ndani!”	Chorus: “Hallo medicine man! To you I have come, medicine man.” “Come in!” “Help me, medicine man, so that I may stay in power, medicine man.” “You, come in!”
“Pita ndani, kijana, pita, ingia.” “Asante!” “Abali <sup>9</sup> ya uko ulikotokea?”	“Come in, youngster, come in, enter.” “Thank you!” “What news do you bring from where you are coming?” “Fine.”
“Nzuri.” “Nimekuona tangu wewe unafikilia kwa mganga kuelekea, na tatizo lako mie nimesalijua.” “Eee?” “Nikisema kweli tawile <sup>10</sup> we itikia. Kuna madalaka wewe anayasikilia.” “Tawile.” “Na hiyo madalaka wengi wayawania.” “Tawile.” “Wewe madalaka hutaki kuachia.” “Umejuaje?” “Tatizo ndogo hiyo nitatua.”	“I have seen you since you were thinking of going to the medicine man, and your problem, I know it already.” “Eee?” “If I’m right, you reply ‘ <i>tawile</i> ’. There is power which you are holding.” “ <i>Tawile</i> .” “And this power – many are striving for it.” “ <i>Tawile</i> .” “You don’t want to give up power.” “How did you know?” “This is a small problem, I will solve it.”

<sup>6</sup> *Be* is the response of women to a call, to signal attention. It is not used by men.

<sup>7</sup> The concept of *mganga* comprises ‘healer’ and ‘magician’.

<sup>8</sup> *Mama* is a term of address used towards women in general.

<sup>9</sup> *Abali* is a dialectal pronunciation of Standard Swahili *habari*. This stylistic device marks the medicine man as an up-country man whose speech is affected by his mother tongue. In this case the pronunciation is that of a Luo, for example *sh* is replaced by *s*.

<sup>10</sup> Zaramo medicine men in Dar es Salaam ask their clients to confirm the information he is giving them about their case by *Tawile* (Swantz 1990: 68).

Kuna vifaa mie nitakuagizia,  
 kwa kazi yako ndiyo tutavitumia,  
 Kaniletee kleti mbili za bia.”  
 “Simpol!”  
 ”Sigara pakti mbili na kibiliti,  
 kitimoto<sup>11</sup> kilo tano losti, umesikia?”  
 ”Aya.”  
 “Machozzi ya samaki ambaye analia.”  
 “Mh!”  
 “Ndevu mbili za Osama akiwa amesinzia.”  
 “Hapana.”  
 “Nazi mbili za nyota yako kuvutia,  
 Kama umeshindwa acha hela nitakutafutia,  
 milioni moja inatosha ya kununulia.”  
 “Poa!”

**Kiitikio:**

Hodi mganga .... x 2

“Vifaa nimepata na dawa nimekutengesea,

Nimeweka kwenye hilizi ii hapa, chukua.  
 Uwe nayo mfukoni popote unapotembea,

utafanikiwa maswala tukizingatia.

Nazi Mtaa wa Kongo<sup>12</sup> ndiyo utakapovunjia  
 saa saba na nusu mchana kama ikitimia.  
 Alafu usisahau kuzikojolea.  
 Kuanzia leo gali marufuku kutembelea,  
 Kampeni ufanye kwa miguu, umesikia?  
 Si ruhusa tena kulala kitandani,  
 ndugu awe mpambe wa kukupigia kampeni.

Mikutano yako yote uyafanyie juani,  
 Wananchi wanayekusikiliza wakae kivurini,

Ila wewe tu ndiyo ukae juani.  
 Tukizingatia haya wewe utafanikiwa.”  
 “Hakuna tabu bwana mimi nimekusikia,  
 masharti yote haya mie nitazingatia.  
 Milioni tano hizi hapa wewe chukua,  
 na naahidi gari mimi ntakununulia,  
 endapo tu madarakani ntabakia, umesikia?”

**Kiitikio x2**

There are some utensils that I will request from  
 you.  
 We will use them for your case.  
 Go and bring me two crates of beer.”  
 “Simple.”  
 “Cigarettes, two packets, and matches,  
 porc meat, five kilos, roasted, have you heard?”  
 “Okay.”  
 “The tears of a crying fish.”  
 “Mh!”  
 “Two beard-hairs of Osama while he is asleep.”  
 “Impossible.”  
 “Two coconuts in order to attract your star.  
 If you are unable [to bring this], leave me money, I  
 will find it for you  
 One million is enough to buy it.”  
 “Okay!”

**Chorus x2**

“I have got the utensils and I have prepared the  
 medicine for you.

I have put it in this amulet here, take it.  
 You must have it always in your pocket wherever  
 you go.

If we are attentive to the requirements, you will be  
 successful.

The coconuts you have to break in Congo Street  
 at half past one o'clock at noon, sharp.  
 And don't forget to urinate on them.  
 From today it is forbidden to go by car,  
 The campaign you have to do on foot, you hear?  
 You are not allowed to sleep in a bed,  
 a brother should be your adjutant who conducts the  
 campaign for you.

At all your meetings you have to stand in the sun,  
 while the citizens who listen to you sit in the  
 shade,

only you have to sit in the sun.  
 If we are attentive to this all, you will succeed.”

“No problem, man, I have understood you,  
 all these conditions I will observe.  
 These five millions here – take them,  
 and I promise that I will buy you a car,  
 If only I stay in power, you understand?”

**Chorus x2**

<sup>11</sup> *Kitimoto* is a slang expression for ‘porc meat’ (for etymology see Reuster-Jahn & Kießling 2006: 135).

<sup>12</sup> A street in Kariakoo, Dar es Salaam.

## No. 2 *Tawile 2 - Joni Woka*

“Mama Juma na wanao, hebu njooni!  
Kuanzia leo sitaki kuwaona humu ndani.  
Kwanza humu ndani nyie mnamtegemea nani?”  
“We, mume wangu!”

“Ah, mimi, eh.  
Ambaye hajapiga. kura humu ndani ni nani?  
Kama wote mmepiga sasa mlimpigia nani?  
Mie kupata kura moja, bwana, haiwezekani.  
Ni aibu, ni aibu kubwa jamani.  
Nimekuwa kama siishi na watu humu ndani.”

“Haya masharti ya mganga, mume wangu  
umeyafuatilia?”  
“We we we we, koma, tena koma, umesikia?  
Habari za mganga humu ndani sitaki kuzisikia.  
Pesa zangu nyingi huyo amenitafunia,  
halafu chochote wala hajanisaidia.  
Tena, kwake sasa hivi mie naelekea,  
Na nikimkuta leo huyu atanitambua.  
Nikifika mimi kwanza nakata halafu nafunua.  
Nikija kufunika mjue nimeshamwua.  
Na nikirudi hapo nyumbani wote mnatimua,  
mmesikia, he?”

### *Kiitikio x2:*

“Tulikupa madaraka kumbe umeyachezea,  
uchaguzi unapofika kwa mganga unaelekea, when the election comes close, you go to the medicine man.  
Shauri yakoooo!  
Oh, shauri yako, hicho kiini macho!  
Na ulie baba.”

“Kalibu, kalibu, kalibu, mesimiwa<sup>13</sup>.”  
“Hakuna cha mheshimwa, wala cha mshtakiwa!  
Nasema leo hii utanitambua!  
Kwanza wewe siyo mganga, mimi nimegundua,

Wewe mwanga tu unaniwangia.”  
“Wee! Ishia apo apo!  
Unataka nikugeushe mlupo?<sup>14</sup>  
Kweli mkuki kwa nguluwe ndiyo tamu,  
ila ni chungu sana kwa binadamu.  
Wewe uliomba wananchi kazi,  
na wananchi wakakupa hiyo kazi,  
ukaona kazi hukufanya kazi,

Ahadi zako ukawa huzitekelezi,  
Tulikupa madaraka ukalala uzingizi,  
hukuwajibika ukategemea hii ilizi,

ukaamini mimi nitakusaidia,  
wakati mimi pia ni Mtanzania  
ambaye maendeleo nayalilia.  
Yaliyokupata wewe umejitakia.  
Ungetimiza ahadi madarakani ungebakia.

Mama Juma, with your children, come here!  
From today onwards I will not see you in here any more.  
First of all, on whom do you depend in this house?”  
“On you, my husband!”

“Aha, on me, eh.  
Who is the one in this house who has not voted?  
And if you all have voted, who has voted for me?  
For me it is impossible to get only one vote, man.  
It’s a shame, it’s a big shame, people.  
It appears as if I don’t live with people in here.”  
“Those conditions of the medicine man, my husband, did  
you follow them?”

“You, you, you, you, shut up, again, shut up, you hear?  
I don’t want to hear about the medicine man inside here.  
He has chewed much of my money,  
and then he didn’t help me with anything.  
I tell you, I will go to him on the spot,  
And if I meet him today, he will know me.  
When I arrive I will directly throw him to the ground.  
When I have overwhelmed him, know I have killed him.  
And when I come back here, you all have to go away,  
have you heard me, he?”

### *Chorus x2:*

“We gave you power, but you played with it,  
when the election comes close, you go to the medicine man.  
It’s your own fault!  
Oh, your own fault, this is a conjurer’s trick!  
Now just cry, father.”

“Welcome, welcome, welcome, Honourable.”  
“There is nothing about “Honourable”, nor about “Accused”!  
I tell you, today you will know me!  
First of all – you are not a medicine man, I have realized  
that.

You are just a sorcerer, who is bewitching me.”  
“Youuu! Stop right here!  
Or do you want me to turn you into a girl?  
It’s true, the spear is sweet for a pig,  
but very bitter for the human.  
You asked the citizens to give you work,  
and the citizens gave you that work,  
and then you realized that it was real work, therefore you  
did not work.

And so you did not fulfill your promises.  
We gave you power, but you slept.  
you didn’t act responsibly, instead you relied on this  
amulet,

believing that I would help you,  
while I’m also a Tanzanian  
who is longing for progress.  
What has befallen you is self-inflicted.  
Had you fulfilled the promises, you would have stayed in  
power.”

<sup>13</sup> As in *Tawile* (part 1) the medicine man’s pronunciation is that of an up-country man, presumably of Luo origin.

<sup>14</sup> *mlupo* is a slang expression meaning ‘young woman easily laid’ (Reuster-Jahn & Kießling 2006: 153).

**No. 4 *Mrisho*<sup>15</sup> – Ngwair**

Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!  
 Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!

Mrisho njoo nimekuita mdogo wangu,  
 nikueleze yaliyo moyoni mwangu.  
 Siwezi kukuficha,  
 kwani wewe ni ndugu yangu.  
 Unakumbuka baba nyumba hii aliniachia  
 na mambo mengi kuhusu nyumba kanihusia.  
 Yote hayo mie nimeyafuatilia,  
 si umeona mafanikio tuliyojipatia?  
 Ila kaka yako Benja sasa hivi nimeugua  
 inanibidi kuondoka kwenda kujitegemea.  
 Mrisho, nyumba, nyumba nakuachia,  
 na nitakayokuambia,  
 Mrisho, naomba zingatia.  
 Nyumba hii, bwana, ina wapangaji watatu,  
 hawa walikuwepo tangu enzi ya baba yetu.  
 Ni Ujinga, Maradhi na Umaskini wetu,  
 hawa ndiyo kikwazo cha nyumba yetu,  
 wanaokwamisha maendeleo ya nyumba yetu,  
 Kuwa makini sana, Mrisho, na hawa watu,  
 wabane! Wabane wasiharibu nyumba yetu.

Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!  
 Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!

Nilishakumbuka kupunguza madeni,  
 ila wewe usiache kukusanya kodi ndani.  
 Tena simamia, simamia kwa makini,  
 ikusaidie kurekebisha humu ndani.  
 Ona jinsi elimu ilivyo duni,  
 Ujinga pia naye aondoke humu ndani.  
 Madawa hospitalini hayapatikani,  
 maradhi yametuandama sana humu ndani,  
 yote hayo kwa sababu ya Umaskini.  
 Sasa hivi kamwoa Rushwa kamleta ndani.  
 mbane Rushwa asitawale humu ndani,  
 ili nyumba yetu isiwe masakani.  
 ila siyo siri, Mrisho nakuamini,  
 kwa sababu ulishapitia jeshini.  
 Nakushauri umpe notisi Umaskini,  
 yeye ndiye kikwazo cha maendeleo.  
 Pia usiwasahau hawa wadogo zako,  
 hawa si taifa la kesho, ni la leo!  
 Uwapatie hila ya kukwea maisha yao.

I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!  
 I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!

Mrisho, come here, I have called you, my younger brother,  
 In order to explain to you what is in my heart.  
 I can't hide it from you,  
 since you are my brother.  
 You remember that father<sup>16</sup> has left this house to me,  
 and he gave me many instructions regarding the house.  
 I have followed all of them,  
 and haven't you seen the achievements we have made?  
 But now, I, your brother Benja<sup>17</sup>, I have fallen ill,  
 I have to leave and rely on myself.  
 Mrisho, the house, the house, I leave it to you,  
 and what I will tell you,  
 Mrisho, please, take note of it.  
 This house, man, has three tenants,  
 who have been here since the time of our father.  
 They are our Ignorance, Diseases, and Poverty,  
 it's them who are the obstacle for our house,  
 who impede the development of our house.  
 Be very serious, Mrisho, about these people,  
 clamp down on them! Clamp down on them lest they destroy our house.

I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!  
 I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!

I have already managed to reduce the debts,  
 however, do not abandon the collection of taxes.  
 Furthermore, supervise, supervise it attentively,  
 so that they [the taxes] may help you to do make improvements here inside.  
 See how mediocre education is,  
 so Ignorance should leave this house.  
 In the hospitals there is no medicine available,  
 we are constantly afflicted with diseases,  
 and all this is because of Poverty.  
 Only recently he has married Corruption and has brought her in here.  
 Clamp down on Corruption, so that she doesn't rule here inside,  
 so that our house doesn't become her dwelling place.  
 And it is not a secret, Mrisho, I trust you,  
 because you have gone through the army.<sup>18</sup>  
 I advice you to give notice to Poverty,  
 'cause he is an obstacle for development.  
 And don't forget your younger siblings,  
 they aren't the nation of tomorrow, but of today!  
 Give them the know-how to master their lives.

<sup>15</sup> Mrisho is the second name of the then presidential candidate of the CCM, Jakaya Mrisho Kikwete.

<sup>16</sup> Baba ('father') is an epithet of the first president of Tanzania, Julius Kambarage Nyerere, who died in 1999.

<sup>17</sup> Benja refers to the former president of Tanzania, Benjamin Mkapa (1995- 2005).

<sup>18</sup> This refers to the fact that Jakaya Mrisho Kikwete has been a member of the army.

Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe maskini –Mrisho!  
 Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!

Tangu baba yetu hajaondoka duniani,  
 alipenda sana kudumisha amani.  
 Kwa kumwenzi baba, Mrisho, linda amani.  
 Mila na desturi ya nyumba hii ni amani.  
 Pinga sana ubaguzi wa kabila na dini.  
 Zingatia kuishi vizuri na majirani,  
 shirikiana<sup>19</sup> nao kuleta maendeleo mtaani,  
 Likitokea tatizo basi saidianeni,  
 kama baba yetu alivyowasaidia zamani.  
 Ila nakusih sana kuwa nao makini  
 kwani hujui rafiki au adui ni nani.  
 ehee, Mrisho kuna kitu nimekumbuka,  
 baba alituachia tochi unaikumbuka?  
 Basi kila mwaka humu ndani zunguka!  
 Tumia tochi hili kila chumba kumulika,  
 uyafichue mabaya na maovu yaliyofichika.  
 Usijali, mungu atakusaidia,  
 na malengo yako yote atatimia!

Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!  
 Nakukabidhi nyumba hii – Mrisho!  
 Yenye utulivu na amani – Mrisho!  
 Isimamie kwa makini –Mrisho!  
 Na uondoe umaskini –Mrisho!

I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!  
 I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!

Before our father had left this world,  
 he liked to maintain peace very much,  
 So, in order to revere father, Mrisho, guard peace.  
 The morals and customs of this house are peace.  
 Strongly oppose ethnic and religious discrimination.  
 Think of living well with your neighbours,  
 cooperate with them and bring development to the neighbourhood.  
 If there occurs a problem, help each other,  
 like our father helped them in the past.  
 However, I beg you, observe them closely,  
 because you don't know who is a friend and who is an enemy.  
 Ehee, Mrisho, there is another thing coming to my mind,  
 father has left us the torch<sup>20</sup>, do you remember it?  
 So, every year go around with it inside here,  
 and use it to illuminate every room,  
 in order to discover the bad and rotten things that are hidden there.  
 Don't worry, God will help you,  
 and all your goals He will achieve!

I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!  
 I hand this house over to you – Mrisho!  
 It is calm and peaceful – Mrisho!  
 Preside over it attentively – Mrisho!  
 And remove poverty – Mrisho!

<sup>19</sup> Standard Swahili: shirikiana.

<sup>20</sup> This refers to the Uhuru Torch, a national symbol of Tanzania which symbolises freedom and light. It was first lit on top of mount Kilimanjaro in 1961, symbolically to shine the country and across the borders to bring hope where there is despair, love where there is enmity and respect where there is hatred. Yearly there is the Uhuru Torch race, starting from different prominent places in the Republic.



## No. 5 *Rais wa Bongo – Soggy Doggy*

Ah, ah ah aha ah  
 Nane noni, Chifu Rumanyika.  
 Kiutani utani.  
 Maana amekuwa raisi  
 Serikalini Soggy Doggy ndo kama bosu,  
 kama sinema jiulize itakwishaje?  
 Miaka yangu mitano serikali itakwendaje?  
 Ahaaaa  
 Watu wengi wajiuliza ntakapokuwa raisi  
 wizara nani ataongoza?  
 Haijulikani kati ya Jay, GK, Mwana FA,  
 nani waziri mkuu.  
 Kila mtu cheo hiki atatamani,  
 ili bungeni apate kushika usukani.  
 Msiulize kuhusu wizara ya madini.  
 Hiyo ni ya Feruzi nilimpa ndotoni.  
 Wizara mpya ya burudani,  
 hiyo mpaka hivi sasa najiulza nimpe nani?  
 Ni Abdul a.k.a Dully Sykes,  
 au Ali Tekuni a.k.a Mchizi Moxx?  
 Ndio Domo mazingira,  
 Mr. II atakuwa wa biashara.  
 Wizara ya mambo ya ndani itakufaa Mr. Blue,  
 kwanza wewe bado mtoto namteua Fid Q.

### ***Kiitikio x2:***

Nimchague nani?  
 Nimpe uongozi atawale kisanii?  
 Atoe mchango kwa jamii,  
 awe kinara bora wa wasanii.

“Soggy, niteue mimi kwa mali asili au utalii.”  
 A’a, haikufai ni Mike T na Jay Dee.  
 Kuhusu mambo ya nje ni TID na Ray C.  
 Nitaanzisha wizara ya pombe hapo nitamweka  
 Suma G.

Dokii, Caz T wizara itakuwa nanii.  
 Mawasiliano na uchukuzi  
 itamfaa Mac to Be.  
 CzG, Suma Lee, Mez B nafikiria.  
 Na nikiwa raisi ati nyie nitawabania  
 Juma na Ngwea  
 A’a, kama mnalia,  
 katiba na sheria wizara nitawapatia.  
 Wizara ya michezo imezidi kuvurugwa,  
 Mkoloni nitapatia kila mechi tutashinda.

Kuna wizara nyingine naziona kama mtaji  
 hasa hii ya fedha inasemekana ina ulaji.

Ah, ah ah aha ah  
 Nane noni, Chief Rumanyika<sup>21</sup>.  
 Just joking.  
 I mean, he has been [elected] president,  
 Soggy Doggy, as boss of the government,  
 like in the cinema, you may ask yourself “how will  
 it end?”  
 My five years – how will the government go?  
 Ahaaaa.  
 Many people are asking themselves, if I would be  
 president,  
 who would lead the ministries?  
 It’s not known, who among Jay, GK or Mwana FA  
 would be prime minister.  
 Everybody covets this position,  
 in order to hold the steering wheel in parliament.  
 Don’t ask about the ministry of minerals.  
 This will be Feruzi’s, I have dreamt I gave it to him.  
 The new ministry of entertainment,  
 up to this moment I’m still thinking of whom I should  
 give it.

Is it Abdul a.k.a. Dully Sykes,  
 or Ali Tekuni a.k.a. Mchizi Moxx?  
 Of course Domo for environment.  
 Mr. II will be the one for trade.  
 The ministry of internal affairs will suit you, Mr. Blue  
 but since you’re still too young, I’ll give it to Fid Q.

### ***Chorus x2:***

Whom should I choose?  
 Whom should I give the leadership to rule artfully?  
 To make a contribution to society,  
 and be a good leader of the artists.

“Soggy, choose me for natural resources or tourism”  
 A’a, it doesn’t fit you, it’s for Mike T and Jay Dee.  
 As for external affairs it will be TID and Ray C.  
 I will start a new ministry for liquor, where I will  
 put Suma G.

Dokii, Caz T, their ministry will be thingy.  
 Communications and transport  
 will suit Mac to Be.  
 I’m thinking of CzG, Suma Lee, Mez B.  
 And if I would be president I would skimp you,  
 Juma and Ngwea.  
 And if you cried,  
 I would give you the ministry of constitution and law.  
 The ministry of sports has become too messed up,  
 I would give it to Mkoloni, so we would win every  
 match.

There are other ministries which I consider as capital,  
